### Matibabu

Wakati wa taratibu ya pendekezo, unaweza kupewa matibabu kama dawa na una chaguzi kulikubali au kulikataa. Hata hivyo, ukilikataa na wafanyakazi wanaona matibabu ni lazima kuokoa maisha yako au kukuzuia kusababisha madhara ya kimwili kwa wewe mwenyewe au wengine, ndipo matibabu yanaweza kupewa bila ruhusa yako. Hii inaitwa matibabu ya akili ya dharura.

### Haki zako wakati unapopendekeza

- Una haki ya kupokea maelezo kuhusu haki zako, kupata majibu kwa maswali yako na kufahamishwa kabisa kuhusu matibabu yoyote yanayotolewa kwako
- Ukiwa unafungwa, una haki kuweza kuwasiliana na watu pamoja na mtunzaji na mwanafamilia wako.
- Una haki za ufaragha na usiri
- Una haki kuomba msaada kutoka Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili. Hii ni huduma bure na huru (s: 1800 999 057).
- kama hufurahi kuhusu jambo fulani, una haki kutoa malalamiko kwa huduma ya afya ya akili. Unaweza pia kulalamika kwa Ofisi ya Malalamiko ya Huduma za Afya na Ulemavu (HaDSCO) (s: 1800 813 583).

### Maelezo zaidi

Maelezo katika brosha hii inahusisha masheria ambayo yamo Sheria ya Afya ya Akili 2014. Maelezo kuhusu Sheria hii imefupishwa katika seti ya brosha zifuatazo:

- Kupendekezwa kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi
- Maagizo ya matibabu kwa mgonjwa aliyelazwa hospitalini
- Maagizo ya matibabu ya jamii
- Maelezo kwa wagonjwa wa hiari
- Kupokea matibabu kwa ugonjwa wa akili
- Maelezo kwa watu wanaosaidia kibinafsi
- Watu walioteuliwa: Jinsi ya kuteua na maana kwake

### Brosha zingine zinapatikana kutoka:

- •Baraza ya Afya ya Akili
- Huduma ya Utetesi wa Afya ya Akili
- Kituo cha Sheria ya Afya ya Akili.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Sheria ya Afya ya Akili 2014 na nyenzo zingine, angalia tovuti ya Tume ya Afya ya Akili: www.mhc.wa.gov.au au pigia simu (08) 6272 1200

This document can be made available in other languages and alternative formats on request.

Published by the Mental Health Commission (2015)

Government of **Western Australia**
**Mental Health Commission**

# Kupendekeza kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi



Pendekezo la Fomu 1A ni agizo chini ya Sheria ya Afya ya Akili 2014 kwa wewe kupata uchunguzi na mtaalum wa magonjwa ya akili.

Brosha hii inakupa maelezo kuhusu haki zako ni nini na unachoweza kutazamia kama wewe upo na pendekezo ya Fomu 1A.

# Kupendekeza kwenda kwa mtaalum wa magonjwa ya akili kwa uchunguzi

**Pendekezo la Fomu 1A** ni tofauti na pendekezo la kawaida kufanywa na GP kwenda miadi na mtaalum. Pendekezo la Fomu 1A ni agizo chini ya Sheria ya Afya ya Akili 2014 kwa wewe kuwa na uchunguzi na mtaalum wa magonjwa ya akili.

Kama upo na pendekezo la Fomu 1A ni kwa sababu daktari au mweledi wa afya ya akili mwenye sifa sana, inayoitwa 'mweledi wa afya ya akili mwenye mamlaka', amekupima na anafikiria kwamba unahitaji matibabu yasiyokusudiwa ya magonjwa wa akili. Mtaalum wa magonjwa wa akili pekee anaweza kuamua kwa vyovyote vile unahitaji matibabu yasiyokusudiwa ya magonjwa wa akili kwa hiyo daktari/mweledi amejaza Fomu 1A kukupendekeza kwenda mtaalum wa magonjwa wa akili kwa uchunguzi.

## Maana ya pendekezo ni nini?

Pendekezo la Fomu 1A inafaa kwa siku 3. Linaweza kurefusha kuwa siku 6 katika maeneo yasiyo miji.

Kuwa upo na pendekezo la Fomu 1A kuna maana kwamba lazima uende kwa uchunguzi na mtaalum wa magonjwa ya akili pale mahali panapotajwa katika pendekezo. Ikihitajika, daktari/mweledi anaweza kukufunga kuhakikisha kuwa unafika mahali pa uchunguzi. Anaweza pia kupanga afisa wa usafiri au afisa wa polisi kukuchukua kwa uchunguzi kama hakuna njia nyingine za salama.

Mara unapowasili kwa mahali pa uchunguzi, huwezi kuondoka mpaka mtaalum wa magonjwa ya akili amekuchunguza, (isipokuwa unasubiri kwa zaidi ya masaa 24, ndivyo unaweza kuondoka).

## Uchunguzi na mtaalum wa magonjwa ya akili

Mtaalum wa magonjwa ya akili atakuchunguza kwa njia ya kuongea nawe na kuuliza maswali. Ikihitajika, mfasiri atatumiwa. Katika baadhi ya maeneo ya pori, uchunguzi unaweza kufanyikiwa juu ya kiungo cha video.

Ukiwa mtu wa Asili au Mtu wa Visiwa vya Torres ya Mlango Bahari, uchunguzi unaweza kufanyikiwa na msaada wa mfanyakazi wa afya ya akili wa Asili au Mtu wa Visiwa vya Torres ya Mlango Bahari, na/au wajumbe muhimu wa jamii yako.

Katika uchunguzi mtaalum wa magonjwa ya akili atafikiria vigezo, ili kuamua kwa vyovyote vile au sio unahitaji matibabu yasiyokusudiwa:

- Je, una ugonjwa wa akili unaohitaji matibabu?
- Kuna hatari ya maana kwako mwenyewe au kwa mtu mwengine kama hupati matibabu?
- Una afya nzuri ya kutosha kuweza kuamua uamuzi kuhusu matibabu?
- Kuna njia yenye mipaka kidogo zaidi ya kukupa matibabu badala ya matibabu yasiyokusudiwa?

## Maamuzi yaliyoamuliwa na mtaalum wa magonjwa ya akili

Baada ya kuongea nawe na kufikiria vigezo, mtaalum wa magonjwa ya akili anaweza kuamua mojawapo ya maamuzi yafuatayo:

- Huhitaji kuwa mgonjwa asiyekusudiwa na lazima uruhusiwe kuondoka. (Hata hivyo unaweza kukubali kupata matibabu kama mgonjwa wa hiari).
- Unahitaji kuwa mgonjwa asiyekusudiwa na unahitaji kupokea matibabu hospitalini. Mtaalum wa magonjwa ya akili atafanya agizo la matibabu ya mgonjwa aliyelazwa (Fomu 6A au 6B) na utalazwa hospitalini.
- Unahitaji kuwa mgonjwa asiyekusudiwa lakini huhitaji kuwemo hospitalini na unaweza kutibiwa katika jamii. Mtaalum wa magonjwa ya akili atafanya agizo la matibabu ya jamii (Fomu 5A) na utafahamishwa juu ya muda na mahali pa miadi yako ya kwanza.

Ikiwa uchunguzi unafanyikiwa katika hospitali inayolaza wagonjwa wasiokusudiwa (tofauti na zahanati au ED), mtaalum wa magonjwa ya akili anaweza kuchelewa kuamua yoyote ya maamuzi ya juu kwa hadi masaa 72 kuanzia wakati ulipokuingia hospitalini, ili uchunguzi wa ziada unaweza kutokea.

Mtunzaji wako, mwanafamilia wa karibu au mtu mwengine wa kusaidia kibinafsi atajulishwa uamuzi wowote unafanyikiwa na mtaalum wa magonjwa ya akili.

